

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA

03 MEI, 2018



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA – TAREHE 03 MEI, 2018

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima nchini kwa kipindi cha Mwaka ulioishia 31 Desemba, 2016 (*The Annual Insurance Market Performance Report for the year ended 31st December, 2016*).

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

172. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

- (a) Je, Serikali inazo takwimu za kuaminika za Vijana waliohitimu Vyuho mbalimbali ambao hawajaweza kujajiri au kuajiriwa;
- (b) Je, ni Taaluma zipi zina fursa nyingi na zipi zina fursa chache za kujajiri au kuajiriwa baada ya kuhitimu;

(c) Je, kwa kipindi cha miaka mitatu (3) iliyopita ni ajira ngapi zilipatikana.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

173. MHESHIMIWA JOHN WEGESA HECHE (TARIME VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mazingira ya ufundishaji kwa Walimu walio wengi nchini ikiwemo Wilaya ya Tarime yamekuwa sio rafiki ambapo Walimu wamekuwa wakibebeshwa mzigo wa gharama za vifaa vya kufundishia kama maandalio ya somo, chaki n.k:-

Je, matumizi haya yatarekebishwaje katika mfumo huu wa elimu bure ulioanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

174. MHESHIMIWA MUSSA BAKARI MBAROUK (TANGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Tafiti zinaonyesha Watoto njiti Tanzania wanapoteza maisha wakiwa chini ya miaka 5:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani mahsusi kupambana na tatizo hili na kuhakikisha Watoto njiti walio hai wanakuwa bila matatizo;

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu kwa Watanzania juu ya sababu zinazosababisha Watoto kuzaliwa njiti.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**175. MHESHIMIWA LOLESIA JEREMIA
BUKWIMBA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Ni Sera ya Taifa kuwawezesha Wavuvi ili wafanye shughuli zao kwa tija:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha Wavuvi katika ukanda wa Ziwa Victoria.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

176. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alipotembelea Itigi alitoa ahadi ya kusaidia mradi wa maji katika Mji wa Itigi:-

- Je, Serikali imetekeleza kwa kiasi gani ahadi hiyo.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**DODOMA
03 MEI, 2018**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**